HABARI KITAIFA

# Wafugaji Ngorongoro wataja matakwa kuhamia Handeni

Na Godfrey Mushi, NGORONGORO

WAKATI uandikishaji wa kaya zilizo tayari kuhama katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ukiendelea, wananchi wa jamii ya kifugaji ya Kimasai, wametaja matakwa muhimu wanayotaka yatekelezwe haraka na serikali, baada ya kuamua kuwahamishia Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.

Matakwa hayo ni kuwapo shule ya msingi, zahanati, maji, umeme, barabara na kufanyika haraka maandalizi ya umilikishaji wa hatimiliki za ardhi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakazi wa Ngorongoro, akiwamo Ngeresai Mathayo, mkazi wa Kata ya Misigyo, alisema ingawa yeye hajajiandikisha bado, lakini kama anakopelekwa kuna shule, zahanati na maji, yuko tayari kuishawishi familia yake kuondoka.

"Serikali ikituambia huko ninakokwenda kuna dispensary (zahanati), shule ya msingi na sekondari, ambayo watoto wangu watasoma, hakuna tatizo, naenda Handeni.

"Nataka niwe na mahali pa kuishi, nataka niwe na shamba la kulima na mahali mifugo yangu itaishi, kwa sababu nategemea mifugo. Huu udongo au ardhi, ndiyo mafuta yetu na tegemeo la uchumi wetu wafugaji."

Aidha, William Leina, Mkazi wa Kitongoji cha Ngereiyani, Kijiji cha Osinoni, Kata ya Kakesio alisema, "Tunaiomba serikali kuweka bayana mambo ambayo yamekuwa yakipigiwa kelele, wakati wa utekelezaji wa zoezi hili.

"Kuna kitu tunataka kujua kama maji, afya na elimu katika eneo hilo la Msomera vipo? Serikali isikae kimya, itoe taarifa kila mara kuhusu hatua iliyofikia katika utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii," alieleza Leina.

Pia, Damiani Huho, Mkazi wa Kimba, Kijiji cha Kayapus, Kata Ngorongoro, aliomba serikali ifanye haraka kukamilisha taratibu za uwekaji wa huduma muhimu za jamii ili walio tayari kuondoka kwa hiari, wakaanze kufanya shughuli za uchumi kwa uhuru na upana zaidi, badala ya kuwaacha wenye utayari kushawishiwa na wasiotaka kuhama.

"Nina washawishi watu wa Ngorongoro, ambao hawana hiyo hamasa ya kutaka kuondoka au wanashawishiwa na baadhi ya watu, watumie hii fursa vizuri, maana yake hii fursa haitajirudia.

"Baadaye wakishindwa kuitumia vizuri wenyewe watajuta. Kwa hiyo ni heri watumie fursa hii wafanye maamuzi yao kwa hiari yao ili waweze kubadilisha maisha na uchumi wao kutokana na nchi inavyokwenda."

Vilevile, Paulo Olemurua, mkazi wa Kijiji cha Esere, Kata ya Alaitole alisema: "Tunakuomba Rais Samia Suluhu Hassan, utupeleke mahali pazuri. Maendeleo ni vitu vinne, elimu, maji, barabara na umeme; na sehemu tutakayoishi iwe na usalama. Shule ipo na serikali iko inatulinda sisi. Wekeni ulinzi wa kulinda sisi, hospitali na shule watoto wetu wanaenda kusoma huko.

"Naomba ututoe Ngorongoro mapema kabla kiangazi hakijaingia, kwa sababu mifugo haitaki kuitoa hapa kupeleka kule hatujui tupite nayo wapi tusigombane na wakulima maana sisi ni wageni. Nafuu kuwahi kuondoka, wakati huu wa masika."

Hadi kufikia juzi, mamia ya wananchi waliojiandikisha kukubali kuondoka ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wanatoka katika Kata za Enduleni, Kakesio, Aleilai, Alaitole, Nainokanoka, Olbalbal, Misigyo, Engaresero, Olorieni na Kata ya Ngorongoro.

Naye, Sara Koromo, Mkazi wa Kata ya Engaresero, alisema kwakuwa wananchi wapo tayari kuhama na kwenda walipotafutiwa na serikali, wanaomba eneo hilo liwe na zahanati ili waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu kufuta huduma afya.

Machi 10, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, baada ya kumaliza kikao chake na viongozi wa mila wa jamii ya Kimasai eneo la Oretei Loongaiki-Marya, kwenye Chuo cha Ufundi Arusha,

Alisema amepokea orodha ya majina ya awali ya kaya 86 zenye watu 453 ambao wamekubali kuondoka kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari, huku wengine wakiendelea kujiandikisha.

Mafanikio hayo yalitokana na mazungumzo ya Waziri Mkuu aliyoyafanya na wadau wa uhifadhi kwenye vikao vilivyofanyika Februari 14 na 17, mwaka huu katika Tarafa za Loliondo na Ngorongoro.

Scanned with CamScanner

# Utafiti kufanyika kupunguza matumizi ya dawa ufugaji kuku

**Na Mwandishi Maalumu, Dodoma**

WATAALAMU wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameandaa miradi miwili ya kutafiti njia mbadala kupunguza matumizi ya dawa katika ufugaji kuku.

Timu ya wataalamu kutoka SUA na Shirika la Kimataifa la Denmark la ICARS, linaloshughulika na afya za wanyama na binadamu jana walikutana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega kumueleza miradi hiyo itakavyotekelezwa nchini.

Akiwasilisha taarifa ya miradi hiyo Mtafiti kiongozi wa miradi hiyo kutoka SUA, Profesa Robinson Mdegela alisema kumekuwa na matumizi makubwa ya dawa hasa antibiotiki kwenye ufugaji wa kuku wa kisasa, ambayo husababisha mabaki ya dawa kwenye nyama na mayai.

"Madhara ya ulaji wa mazao ya kuku yenye mabaki ya dawa ni pamoja na usugu wa vimelea kwenye dawa huku pia mfugaji akitumia gharama kubwa ya kununua dawa ambayo angeweza kuiepuka," alisema Profesa Mdegela.

Alisema wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wataalamu kutoka SUA wameandika maandiko mawili ya miradi ya kutafiti kuhusu uwezekano wa kutumia njia za usafi kwenye mabanda ya kuku na kuichanja mifugo hiyo ili kudhibiti magonjwa.

Ulega alisema miradi hiyo imekuja wakati mwafaka kwa kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika jitihada za kuhamasisha ufugaji wa kisasa kuongeza uzalishaji wenye tija utakaohakikisha usalama wa chakula nchini.

"Nawapongeza wataalamu kwa kuja na miradi hii ambayo inakwenda kutafuta suluhisho la changamoto za matumizi makubwa ya dawa kwa kuku, naomba mkasimamie vyema utekelezaji wa miradi hii ili matokeo yakaonekane kwa haraka na wananchi wawe na uhakika na chakula wanachokitumia," alisema.

Ulega alilishukuru shirika la Kimataifa la ICARS la Denmark kwa kukubali kufadhili miradi hiyo miwili kwa miaka mitatu kuanzia Mei mwaka huu hadi Mei 2025.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo utasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa athari za matumizi hayo ya dawa kwa walaji lakini pia itawapunguzia mzigo wa gharama wafugaji.

Mkurugenzi wa Uendeshaji kutoka Shirika la ICARS, Helle Engslund Krarup aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuruhusu miradi hiyo kutekelezwa nchini.

"Tuna imani ushirikiano huu utafanikiwa na miradi hii itasaidia jamii kubadili namna ya ufugaji wao na pia itasaidia taifa kuona kama kuna haja ya kutunga sera na miongozo ya ufugaji bora wa kisasa," alisema Krarup.

Scanned with CamScanner

ziara ya Waziri wa Uingereza

irikiana na serikali ya

inapungua kama si kutokomezwa kabisa.

wakati katika eneo moja na kuharakisha utoaji huduma.

HABARI LEO UK 16



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akizungumza na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Shirika la ICARS, Helle Engslund Krarup alipokutana naye ofisini kwake mkoani Dodoma jana. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Scanned with CamScanner



ne

sha

ioja na ku-
arasani.
awaweze-
fundishaji
ana na azma
nu nchini.

mbali na
, Mara,
, Rukwa na

u, David
naishukuru
saidia elimu
. Akatoa
ngereza
oletwa zita-

wa Pwani,
ema anashu-
a mradi
nza na
e manufaa

# Serikali yaombwa kuongeza nguvu kudhibiti uvuvi haramu

Na Yohana Shida, Geita

KAMATI ya Usimamizi wa Maeneo ya Fukwe (BMU) wilayani Chato mkoani Geita imeiomba serikali kuongeza nguvu katika kukabiliana na uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira katika Ziwa Victoria.

Kamati hiyo imesema mbali na juhudi wanazoendelea kuzifanya kulinda rasilimali za majini, bado kuna haja ya serikali kuwekeza zaidi ili kuimarisha sekta ya uvuvi.

Mwenyekiti wa BMU wilayani Chato, Bashir Mathias alieleza hayo juzi katika mahojiano maalumu na HabariLEO juu ya mwenendo wa uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za majini.

Bashir alisema mbali na BMU kutimiza majukumu yake kwa kufanya doria za mara kwa mara, bado tatizo la uvuvi haramu limeendelea kujitokeza, hali inayohatarisha uhai wa sekta ya uvuvi.

Alieleza kwamba BMU imebaini kiini cha tatizo ni wavuvi wengi kukosa mitaji na kufanya kazi kwa kutumia vifaa duni, hali inayochangia kulazimika kutumia mbinu chafu zinazoangamiza viumbe wa majini na kuharibu mazingira.

"Sekta ya uvuvi iimarishwe, kwani ndiyo ajira yetu sisi. Inaweza kutusaidia kupata kipato kikubwa kuliko kipato kilichopo sasa hivi, kwa sababu sasa hivi tumekuwa tukifanya maendeleo lakini siyo mazuri," alisema.

Alisema ili elimu inayotolewa kuhusu athari za uvuvi haramu izae matunda ni vyema wavuvi wawezeshwe vitendea kazi kupitia mikopo na pia maofisa uvuvi waongezeke ili kuchagiza ari ya wavuvi kuzingatia kanuni za uvuvi.

Scanned with CamScanner